



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ASASI ZA KIRAIA ZILIZOPATA KIBALI
CHA UANGALIZI NA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA WAKATI WA
UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA KWAHANI**

Zanzibar, 11 Mei, 2024

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 11 Mei, 2024, imetoa vibali (kwa asasi nne za kiraia) vya uangalizi na utoaji wa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Kwahani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar kwa asasi nne za kiraia. Tume imefikia uamuzi huo kwa kuzingatia kifungu cha 85(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024 na kifungu cha 10(1)(g) na (h) vya Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024 na vinaipa Tume jukumu la kualika waangalizi wa uchaguzi, kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo. Orodha ya asasi za kiraia zilizopata kibali cha uangalizi na kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi mdogo wa Ubunge katika jimbo la Kwahani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, imeoneshwa katika jedwali lifuatalo: -


NA.	JINA LA ASASI YA KIRAIA/MTAZAMAJI	KIBALI
1.	Zanzibar Fighting Against Youth Challenges Organization	Uangalizi wa Uchaguzi
2.	Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar	Uangalizi wa Uchaguzi
3.	Jumuiya ya Wasaidizi wa Sheria Wanawake Zanzibar (ZAWOPA)	Elimu ya Mpiga Kura
4.	Shirika la Elimu ya Uraia na Uzalendo	Elimu ya Mpiga Kura

NA.	JINA LA ASASI YA KIRAIA/MTAZAMAJI	KIBALI
	Tanzania "Civic Education and Patriotism Association"	

Aidha, katika utekelezaji wa majukumu yao, asasi hizo zitapaswa kuzingatia Mwongozo wa Watazamaji wa Mwaka 2020 na Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Mwaka 2020 katika kipindi chote cha uchaguzi huu mdogo.

Tume inatumia fursa hii kuzipongeza asasi zote za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na uangalizi. Vile vile, Tume inazikumbusha asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kuzingatia ratiba ya utoaji wa elimu ya mpiga kura iliyotolewa na Tume. Pia, asasi za kiraia zinapaswa kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi chote cha uchaguzi. Aidha, Kibali cha uangalizi kitatumika kipindi chote cha uchaguzi huu mdogo na kibali cha kutoa elimu kitatumika kuanzia tarehe 24 Mei, 2024 hadi tarehe 07 Juni, 2024.

Imetolewa na:



Kailima, R. K.
MKURUGENZI WA UCHAGUZI